

SAUTI YA TSC

TOLEO NA. 30 JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC) AGOSTI 2023

WAZIRI KAIRUKI ATOA MAAGIZO KUMALIZA CHANGAMOTO ZA WALIMU



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Mhe. Angellah Jasmine Kairuki akitoa hotuba ya kufungua mafunzo ya Mfomo wa Usimamizi wa Taarifa za Watumishi ujulikanao kama Human Capital Management Information System (HCMIS) yaliyowahusisha watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ngazi ya wilaya na Maafisa Utumishi kutoka Halmashauri zote nchini tarehe 05 Julai, 2023 jijini Dodoma.

MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz

WATENDAJI TSC, HALMASHAURI SAIDIENI SERIKALI KUTIMIZA AZMA YAKE YA KUMALIZA MALALAMIKO YA WALIMU

Serikali imejipanga kumaliza kero na malalamiko mbalimbali yanayowakabili walimu kwa kuhakikisha kila mwalimu anapatiwa haki yake kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu za kiutumishi.

Miongoni mwa kero kubwa ambazo Serikali imejipanga kuzimaliza ni kucheleweshwa kupandishwa vyeo, kupandishwa madaraja bila kuzingatia utaratibu kitu kinachosababisha kutofautiana kwa vyeo kwa walimu wa kundi rika moja (walioanza kazi pamoja na wenye sifa sawa) na kujirudia kwa madaraja (mwalimu kupandishwa cheo katika daraja lile lile alionalo).

Malalamiko mengine ni walimu wanaopanda vyeo pamoja kuidhinishiwa barua za kupanda vyeo kwa tarehe tofauti kwa sababu za kimfumo, kucheleweshwa kubadilishiwa cheo baada ya kujiendeleza kielimu pamoja na madai ya malimbikizo ya mishahara, likizo na uhamisho.

Serikali kupitia Mawaziri wake, Mhe. Angellah Jasmine Kairuki (TAMISEMI) na Mhe. George

Simbachawene (UTUMISHI) kwa nyakati tofauti wameelekeza watendaji wa Tume ya Utumishi wa Walimu na Maafisa Utumishi wa Halmashauri kukusanya taarifa za walimu wote ambao hawajapandishwa vyeo kwa muda mrefu ili waweze kushughulikiwa, kuingiza madai ya walimu ya mishahara kwenye Mfumo wa Watumishi (HCMIS) na pamoja na kufuatilia madai yote ya likizo na uhamisho ili yalipwe.

Ili kufikia azma hiyo, ni lazima watendaji waliopewa dhamana ya kushughulikia masuala hayo kufanya kazi hiyo kwa umaniki na uadilifu ili kuhakikisha kila mwalimu mwenye changamoto taarifa zake zinafika sehemu husika ili hatua ziendelee kuchukuliwa.

Hivyo, ni wito wetu kwa watendaji wa TSC na Maafisa Utumishi wa Halmashauri kufanya kazi hiyo kwa weledi ili kila mwalimu mwenye changamoto aweze kufikiwa na mwisho wa zoezi hilo malalamiko yote ya walimu yawe yamemalizika.

BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti

Paulina M. Nkwama

Wajumbe

Richard L. Odongo
Revocatus P. Misonge
Mectildis F. Kapinga
Lameck S. Mbeya
Zachary A. Dida
Fatuma I. Muya

Mhariri Mkuu

Gerard J. Chami


Mhariri

Adili J. Mhina

Msanifu Kurasa

Lucas G. Ogunde

KATUNI



TSC

Wasiliana nasi kwa Simu: +255 782 366 622 & +255 735-255238 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz
Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, S.L.P 353, DODOMA.



Ofisi ya Rais
Tume ya Utumishi
wa Walimu (TSC)

Maonesho ya NaneNane

2023

“Tunawakaribisha Walimu na wadau kutembelea mabanda yetu kwa ajili ya kupata huduma mbalimbali”

Viwanja vya
John Mwakangale

Viwanja vya
Nanenane

Mbeya ●●● Dodoma

Karibu
TUKUHUDUMIE

Mwl. Paulina M. Nkwama, *ndc*
Katibu, Ofisi ya Rais -TSC



Tume Utumishi wa Walimu Tanzania



www.tsc.go.tz

WAZIRI KAIRUKI ATOA MAAGIZO KUMALIZA CHANGAMOTO ZA WALIMU

Na Mwandishi wetu – Dodoma.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Kairuki amewaagiza maafisa utumishi na Makatibu Wasaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), kuhakikisha wanafuatilia walimu ambao hawajapandishwa vyeo kwa muda mrefu ili waweze kushughulikiwa. Pia, ameagiza kuhakikishwa kuwa madai ya malimbikizo ya mishahara ya Walimu wote yanaingizwa kwenye Mfumo wa Watumishi (HCMIS) na orodha iwasilishwe OR-TAMISEMI ikiwa ni pamoja na kufuatiliwa madai ya Walimu ya likizo na uhamisho ili wapate stahiki zao kwa wakati.

Kairuki ametoa maagizo hayo tarehe 5 Julai, 2023 wakati akifungua kikao kazi cha Maafisa wa Tume ya Utumishi wa Waalimu (TSC) cha Kuwajengea Uwezo kuhusu Mfumo wa taarifa za Watumishi (HCMIS) katika ukumbi wa PSSF jijini Dodoma.

Vilevile, Waziri Kairuki amewaelekeza watendaji hao kufanya kazi kwa kushirikiana na kuacha mivutano wakati wa kutoa huduma ili walimu wasipate usumbufu wakati wa kuhudumiwa.

Kiongozi huyo pia aliwasihii watendaji hao kuwa na lugha nzuri na kuacha tabia ya kuwanyanyasa walimu jambo ambalo linapunguza morali ya kufundisha wanafunzi.

“Naomba muende mkawe na mawasiliano mazuri katika

utendaji wenu wa kazi ikiwemo kutumia lugha za staha kwa walimu pale wanapoleta changamoto zao,” alisema.

Kwa upande wake, Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI, Dk Charles Msonde alisema katika kutafuta namna bora ya kushughulikia na kuyapatia ufumbuzi wa kudumu malalamiko na kero zote za Walimu, mnamo tarehe 21 Juni, 2023 viongozi wa Ofisi ya Rais TAMISEMI, Ofisi ya Rais UTUMISHI na Tume ya Utumishi wa Walimu walifanya kikao cha pamoja ambacho kilitafuta ufumbuzi wa namna bora ya kutatua changamoto za walimu.



Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI) anayeshughulikia elimu, Dkt. Charles Msonde akitoa neno la kumkaribusha Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mhe. Angellah Jasmine Kairuki ili afungue mafunzo ya Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Watumishi ujulikanao kama Human Capital Management Information System (HCMIS) tarehe 05 Julai, 2023 jijini Dodoma.

“Moja ya njia za kutatua changamoto hizo ni kuwapa TSC dirisha la kuingia kwenye mfumo wa HCMIS ili wafanye utekelezaji wa maagizo ya kutatua changamoto za walimu ikiwa ni pamoja na kuunda kikosi kazi cha kuwasikiliza.

Amezitaja changamoto hizo ni upandishaji wa madaraja, kupishana kwa muda wa kupandishwa madaraja bila utaratibu na mfumo wa kubadilishwa vyeo/cheo.

Naye Katibu Mtendaji wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama ameishukuru Serikali kwa kuendelea kuiwezesha Tume hiyo kutekeleza majukumu yake ya kuwahudumia walimu ikiwemo ununuzi wa magari 16 na kompyuta 159.



Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama akitoa neno la utangulizi wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Watumishi ujulikanao kama Human Capital Management Information System (ICMIS) yaliyowahusisha watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ngazi ya Wilaya na Maafisa Utumishi kutoka Halmashauri zote nchini tarehe 05 Julai, 2023 jijini Dodoma.



Washiriki wa mafunzo ya Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Watumishi ujulikanao kama Human Capital Management Information System (HCMIS) yaliyowahusisha watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ngazi ya Wilaya na Maafisa Utumishi kutoka Halmashauri zote nchini tarehe 05 Julai, 2023 jijini Dodoma wakikwa kwenye mafunzo.



Mshiriki wa mafunzo ya Mfumo mpya wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS), Omary Mkuzwili akitoa neno la shukrani kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, Angellah Kairuki wakati wa kufungua mafunzo ya HCMIS tarehe 05 Julai, 2023 jijini Dodoma.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Angellah Jasmine Kairuki (katikati waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya washiriki wa mafunzo ya Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Watumishi yaliyowahusisha watumishi wa TSC ngazi ya wilaya na Maafisa Utumishi kutoka Halmashauri zote nchini tarehe 05 Julai, 2023 jijini Dodoma. Pichani, wa pili kutoka kulia ni Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI anayeshughulikia elimu, Dkt. Charles Msonde na wa pili kutoka kushoto ni Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama.

NANENANE 2023



Tupo tayari kukuhudumia. Tupo viwanya vya John Mwakangale jijini Mbeya na Viwanja vya Nanenane jijini Dodoma.

WAZIRI KAIRUKI AONGOZA UJUMBE WA WATAALAMU WA ELIMU KUFANYA ZIARA NCHINI SINGAPORE

Na Mwandishi wetu - Dodoma

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Angellah Jasmine Kairuki ameongoza ujumbe wa wataalamu wa masuala ya elimu kufanya ziara nchini Singapore kwa ajili ya kupata uzoefu wa namna masuala ya utumishi wa walimu yanavyosimamiwa katika nchi hiyo.

Ziara hiyo iliyofadhiliwa na Mradi wa BOOST ilifanyika Julai 24 – 28, 2023 ambapo ilijikita kuangalia namna Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) nchini inavyoweza kufanya maboresho kwenye utendaji wake katika kushughulikia haki na wajibu wa mwalimu kwenye utumishi wake kwa kujifunza namna nchi nyingine zinavyotekeleza jukumu hilo.

Sababu nyingine ya kujifunza masuala ya usimamizi wa walimu katika nchi zingine ni kuhakikisha kada ya ualimu nchini inakwenda sambamba na mabadiliko mbalimbali yanayotokea ulimwenguni ili kuwezesha wanafunzi kupata elimu inayoendana na maendeleo ya sayansi na teknolojia.

“Mwalimu nchini Tanzania anatakiwa kuwa sehemu ya mageuzi ya kimataifa, na mojawapo ya marekebisho ya kimkakati yanayopendekezwa mara kwa mara, ni kuhakikisha walimu wanapangwa na kusimamiwa ipasavyo,” ilieleza sehemu ya taarifa ya ziara hiyo.

Taarifahiyoiendeleakufafanua kuwa miongoni mwa masuala ya elimu yanavyosimamiwa nchini Singapore ni kuwa elimu ya msingi na Sekondari inatolewa katika shule za serikali pekee. Kila mwaka Idara ya Usimamizi wa



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Angellah Jasmine Kairuki (kushoto) akiwa na Waziri wa Mambo ya Nje na Elimu wa Singapore, Mhe. Dr. Mohamad Maliki Bin Osman.

Rasilimali Watu hufanya tathmini ya utendaji kazi wa kila mwalimu ambapo tathmini hiyo inatumika kama kigezo cha mwalimu kupandishwa cheo.

“Walimu wote wameajiriwa na Wizara ya Elimu nchini Singapore baada ya kumaliza elimu ya ualimu, kupata mafunzo ya miezi sita ya kada ya ualimu na kufuzu kwa usaili. Pia, Baada ya miaka mitatu mwalimu anaweza kuhama na kufanya kazi katika taasisi nyingine na kuendelea kutambuliwa na Chuo cha Ualimu cha Singapore (Singapore Teachers’ Academy),” ilieleza sehemu ya taarifa hiyo.

Jambo jingine katika usimamizi wa walimu nchini Singapore ni kuwa Mwalimu ambaye ametiwa hatiani kwa kosa lolote na kufukuzwa utumishi hawezi kuajiriwa tena katika Utumishi wa Umma. Pia, kiwango cha elimu kwa Walimu wa ngazi zote, ikiwa ni pamoja na elimu ya awali, msingi na sekondari ni kuanzia shahada ya kwanza.

Wakiwa nchini Singapore,

Waziri na ujumbe wake walitembelea Wizara ya Mambo ya Nje na Elimu, Taasisi ya Elimu, Chuo cha Walimu cha Singapore, Shule ya Msingi Noorthshore na Shule ya Sekondari Yusof Ishack.

Wataalamu walioambatana na Waziri Kairuki katika ziara hiyo ni Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia elimu OR – TAMISEMI, Dkt. Charles Msonde, Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais UTUMISHI, Exavier Daudi, Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama na Mkurugenzi wa Idara ya Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu TSC, Mwl. Fatuma Muya.

Wajumbe wengine walioambatana na Waziri Kairuki ni Mratibu wa Mradi wa BOOST TSC, Mwl. Asha Lubuva, Afisa kutoka OR – TAMISEMI, Julius Nyalus, Afisa kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Suleiman Magomba pamoja, Mwalimu Mwandamizi kutoka Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Josephat Luoga pamoja na Afisa kutoka Ubalizi wa Tanzania New Delhi, Fanuel Mathias.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Angellah Jasmine Kairuki (wa kwanza mbele kushoto) akiwa na ujumbe wake pamoja na wanafunzi wa shule ya Msingi Noorthshore nchini Singapore.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Angellah Jasmine Kairuki akiwa na ujumbe wake pamoja na wanafunzi wa shule ya Sekondari Yusof Ishack nchini Singapore.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Angellah Jasmine Kairuki (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Waziri wa Mambo ya Nje na Elimu wa Singapore, Mhe. Dr. Mohamad Maliki Bin Osman (wa tatu kutoka kulia) pamoja na timu ya wataalamu wa elimu kutoka Tanzania wakati wa ziara ya Waziri Kairuki nchini Singapore iliyofanyika tarehe 24 – 29 Julai, 2023.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Angellah Jasmine Kairuki (wa tano kutoka kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na timu ya wataalamu wa elimu katika shule ya Msingi Noorthshore nchini Singapore wakati wa ziara yake nchini hapo iliyofanyika tarehe 24 – 29 Julai, 2023.

**WATAALAMU WA ELIMU NCHINI WATEMBELEA KENYA
KUPATA UZOEFU WA USIMAMIZI WA WALIMU**

Na Mwandishi wetu – Dodoma.

Timu ya wataalamu wa elimu imefanya ziara nchini Kenya kwa lengo la kujifunza namna nchi hiyo inavyosimamia walimu ili kufanya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kuongeza ufanisi katika kutoa huduma kwa walimu.

Ziara hiyo iliyofanyika Julai 25 – 29, 2023 iliongozwa na Naibu Katibu Mkuu kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dkt. Franklin Ndyetabula Rwezimula ambapo wataalamu hao walitembelea – Tume ya Utumishi wa Walimu ya Kenya na Wizara ya Utumishi wa Umma, Jinsia na Ushirikiano (Idara ya Serikali ya Utumishi wa Umma).

Wataalamu walioshiriki katika ziara hiyo iliyofadhiliwa na Mradi wa BOOST ni Mkurugenzi wa Sera na Mipango kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, John Cheyo, kutoka



Mkuu wa msafara wa timu ya wataalamu wa masuala ya elimu kutoka Tanzania waliofanya ziara nchini Kenya tarehe 25 – 29, 2023 ambaye pia ni Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dkt. Franklin Ndyetabula Rwezimula (kushoto) akikabidhi zawadi kwa mwenyeji wake nchini Kenya.

TSC walikuwepo Mkurugenzi wa Kitengo cha Huduma za Sheria, Wakili Richard Odongo, Mkurugenzi Msaidizi wa Ajira na

Maendeleo ya Walimu, Mectildis Kapinga na Mkuu wa Kitengo cha Mipango Ufuatiliaji na Tathmini, Evodia Pangani na kutoka Wizara



Mkuu wa Kitengo cha Mipango Ufuatiliaji na Tathmini kutoka TSC, Evodia Pangani (kushoto) akikabidhi zawadi kwa mwenyeji wake wakati wa ziara ya timu ya wataalamu wa elimu nchini Kenya iliyofanyika tarehe 25 – 29 Julai, 2023.



Mkurugenzi wa Kitengo cha Sheria kutoka TSC, Wakili Richard Odongo (kushoto) akipokea zawadi kutoka kwa mwenyeji wake wakati wa ziara ya timu ya wataalamu wa elimu nchini Kenya iliyofanyika tarehe 25 – 29 Julai, 2023.

WATAALAMU WA ELIMU NCHINI WATEMBELEA KENYA KUPATA UZOEFU WA USIMAMIZI WA WALIMU

ya Elimu Sayansi na Teknolojia alikuwepo Mwalimu Mwandamizi Daudi Minja.

Taarifa ya ziara hiyo imeonesha kuwa wataalamu hao wamepata ujuzi wa masuala mbalimbali ya namna Tume ya Utumishi wa Walimu nchini Kenya inavyosimamia walimu.

“Huduma zote zinazohusu utumishi wa walimu hutolewa na chombo kimoja ambacho ni Tume ya Utumishi wa Walimu ya nchi hiyo. Hivyo, TSC nchini Kenya imesaidia kuondoa changamoto zinazojitokeza kwa walimu kusimamiwa na zaidi ya chombo kimoja,” imeeleza sehemu ya taarifa hiyo.

Tume ya Utumishi wa Walimu nchini Kenya ndiyo Mamlaka ya Ajira na Mwakiri kwa walimu ambapo inatangaza nafasi za kazi, inaajiri, inawapangia walimu vituo vya kazi pamoja na kuwalipa mishahara.

Taarifa imeendelea kufafanua kuwa Tume ya Utumishi wa nchini Kenya ni chombo huru ambacho hakiingiliwi na mamlaka nyingine katika kusimamia Ajira, Maadili na maendeleo ya walimu, ni chombo

kilichoanzishwa chini ya Katiba ya nchi hiyo.

“TSC nchini Kenya ina mifumo madhubuti ya usimamizi wa Utumishi wa Walimu jambo ambalo linaisaidia Tume hiyo kutoa huduma kwa ufanisi. Vilevile, Tume hiyo ipo chini ya Wizara ya Elimu kwa mujibu wa sera ya elimu ya nchi hiyo. Pia, Matumizi ya Mifumo ya kielektroniki katika usimamizi na utoaji wa huduma kwa walimu umeisaidia sana TSC Kenya kutoa huduma kwa ufanisi,” taarifa hiyo imeeleza.

Jambo jingine lililoelezwana timu hiyo ni kuwa TSC Nchini Kenya inasajili na kutoa vyeti vya usaji kwa walimu wote, utaratibu huo ni wa lazima na haijalishi kama mwalimu ameajiriwa au la, ilimradi mwalimu amehitimu ualimu katika chuo cha ualimu au chuo kikuu kinachotambuliwa na Serikali ni lazima asajiliwe na chombo hicho.

TSC Kenya inasimamia Walimu katika Shule za Serikali na za kibinafsi na Mwalimu ambaye ametenda kosa la kinidhamu na kupewa adhabu ya kufukuzwa

kazi hataajiriwa tena katika utumishi huo.

“Mchakato wa kuajiri Walimu na kuwachukulia hatua za kinidhamu unafanyika kwa uwazi. Walimu nchini Kenya hupandishwa vyeo kila baada ya miaka mitatu, vilevile walimu nchini humo wanapatiwa posho ya nyumba kama motisha ya utendaji kazi, hivyo Serikali haina utaratibu wa kujenga nyumba za walimu isipokuwa kwa Walimu Wakuu/Wakuu wa Shule ambao hujengewa nyumba ili kuwa karibu na mazingira ya shule”.

“Kuna mengi ambayo TSC Tanzania inaweza kujifunza kutoka TSC ya Kenya katika utumishi na usimamizi wa Ualimu ili kupunguza mapengo yaliyopo katika utoaji wa huduma za walimu,” ilisisitiza taarifa hiyo.

Taarifa hiyo imehitimisha kwa kueleza kuwa ingawa mfumo wa kisheria uliopo wa utumishi na usimamizi wa Walimu kati ya Kenya na Tanzania unakaribia kufanana, tofauti iliyopo ni njia za utoaji wa huduma.



Picha ya pamoja kati ya timu ya wataalamu wa masuala ya elimu kutoka Tanzania waliofanya ziara nchini Kenya pamoja na wataalamu wa masuala ya usimamizi wa elimu wa Kenya.

WAZIRI SIMBACHAWENE AAHIDI TSC KUPATIWA MAGARI 139



Waziri wa Nchi (Ofisi ya Rais) Menejimenti ya Utumishi wa Umma (OR – UTUMISHI), George Simbachawene (katikati) akipitia nyaraka kabla ya kufunga mafunzo ya Mfumo mpya wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS) tarehe 6 Julai, 2023 jijini Dodoma. Pichani kulia ni Katibu Mkuu wa OR – UTUMISHI Juma Mkomi na kutoka kushoto ni Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama.

Na Mwandishi wetu - Dodoma

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (OR - UTUMISHI), Mhe. George Simbachawene ameahidi kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ili kuongeza ufanishi katika kutoa huduma kwa walimu.

Waziri Simbachawene alitoa ahadi hiyo tarehe 6 Julai, 2023 jijini Dodoma wakati akifunga mafunzo ya Mfumo mpya wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS) yaliyowahusisha watumishi wa TSC ngazi ya wilaya na Maafisa Utumishi kutoka halmashauri zote Tanzania Bara.

Miongoni mwa changamoto zinazoikabili Tume hiyo ni kukosekana kwa vyombo vya usafiri (magari) katika ofisi zote za wilaya, kutokuteuliwa kwa Makatibu wasaidizi wa wilaya, upungufu wa vitendea kazi vya ofisi na upungufu wa vyumba vya ofisi.

Akizungumzia suala la vyombo vya usafiri, Waziri Simbachawene aliahidi watumishi hao atazungumza na Rais Samia Suluhu Hassan kumuomba magari 139 kwa ajili ya ofisi zote za

wilaya ili iwe rahisi kwa watendaji hao kuwafikia walimu.

“Ninaelewa hali yenu ilivyo huko wilayani, ninajua changamoto mnazopitia katika kuwafikia walimu. Kuna maeneo yetu huko ambayo kuyafikia inabidi uwe na gazi nzuri kweli kweli, sasa msipokuwa na magari mtawafikiaje walimu. Agenda hii ninaibeba na nitazungumza na Waziri wa TAMISEMI twende tukamwombe Rais magari 139, ninaamini atatupatia,” alisema Waziri huyo.

Waziri huyo ameeleza kwamba magari hayo yakipatikana sio kwamba yatawasaidia maafisa wa TSC peke yao bali pia yatawasaidia maafisa utumishi kuwafikia watumishi ndani ya hamlasahauri zao ambapo wengi wao ni walimu.

“Magari haya myatumie Pamoja na Maafisa utumishi maana nao hawana magari. Ninyi na Maafisa Utumishi ni lazima muende Pamoja na maafisa utumishi kutatua changamoto za walimu. Kazi yenu mnatakiwa muende kwenye shule msikilize matatizo ya wamumu sio mwalimu anakuja kuwafwata ofisini,”

Kuhusu vitendea kazi, Waziri huyo alisema atahakikisha kila ofosi inapata kompyuta mpakato ili anapokwenda kwa walimu

anatumia kitendeakazi hicho kutunza taarifa za walimu.

Aidha, Waziri Simbachawene alisema atahakikisha Makatibu Wasaidizi wa Tume hiyo wanateuliwa kama inavyoelekezwa katika Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura 448 huku akitoa angalizo kuwa watumishi ambao hawana mwenendo mzuri hawawezi kupata nafasi hizo.

“Ninajua ninyi wenyewe humu mna manung’uniko yenu, zipo changamoto za upandishwaji wa madaraja na masuala ya uteuzi wa Makatibu Wasaidizi. Kabla hamjaenda kumaliza matatizo ya walimu ni lazima tuhakikishe mabo yenu yamekaa sawa ili hata unapokwenda kwa mwalimu uweze kumhudumia vizuri.”

“Katibu Mkuu UTUMISHI ninaomba tuanze na hawa kwanza tuhakikishe matatizo yao yote ya kiutumishi tumeyamaliza. Tutawateua Makatibu Wasaidizi ili hivyo viti vyenu mvikalie sawasawa, tunajua hiki kimekuwa kilio cha muda mrefu lakini sasa tunakwenda kukimaliza. Lakini kabla ya kuwateua lazima tujiridhishe na kila mmoja wenu maana kuna wengine ni wala rushwa, wanyanyasaji kwa walimu na wengine wana tabia ambazo kiongozi hapaswi kuwa nazo, hao hatutawateua,” alisema Waziri Simbachawene.

Kwa upande wake Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama kuwa anamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuiwezesha Tume hiyo kwa rasilimali mbalimbali ili iweze kutoa huduma bora kwa walimu.

Mhe. Rais Kwa kuendelea kuiwezesha tume ya Utumishi wa walimu kwa kuiongeza rasilimali watu na rasilimali fedha na vitu na mafanikio ni pamoja na kuiwezesha tume Kwa kuiongeza bajeti kutoka shilingi bilion 14.8 hadi bilioni 17.2.

Aidha amiongeza kuwa wamefanikiwa kuongezewa watumishi kutoka 482 hadi 574 hili limeenda sambamba na kuiwezesha tume vitendeakazi.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akitoa neno la utangulizi wakati wa kufunga mafunzo ya Mfumo mpya wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS) tarehe 6 Julai, 2023 jijini Dodoma.

Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Juma Mkomi (katikati) akimsikiliza Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama wakati wa kufunga mafunzo ya Mfumo mpya wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS) tarehe 6 Julai, 2023 jijini Dodoma. Upande wa kulia ni Mkurugenzi, Idara ya Usimamizi wa Rasilimaliwatu Serikalini kutoka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ibrahim Mahumi.



Baadhi ya washiriki wa mafunzo ya Mfumo mpya wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS) yaliyofanyika tarehe 4 – 6 Julai, 2023 jijini Dodoma wakikwa katika makundi kwa ajili ya kujifunza mfumo huo.



Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Juma Mkomi (kushoto) akizungumza jambo na Mkurugenzi wa Idara ya Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu wa TSC, Mwl. Fatuma Muya wakati wa kufunga mafunzo ya Mfumo mpya wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS) tarehe 6 Julai, 2023 jijini Dodoma.



Mshiriki wa mafunzo ya Mfumo mpya wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS), Simon Simbujile akitoa neno la shukrani kwa Waziri wa Nchi (Ofisi ya Rais) Menejimenti ya Utumishi wa Umma, George Simbachawene wakati wa kufunga mafunzo hayo tarehe 6 Julai, 2023 jijini Dodoma.



Waziri wa Nchi (Ofisi ya Rais) Menejimenti ya Utumishi wa Umma (OR – UTUMISHI), George Simbachawene (katikati) akiimba wimbo wa Taifa wakati wa kufunga mafunzo ya Mfumo mpya wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS) tarehe 6 Julai, 2023 jijini Dodoma. Wā Pili kutoka kulia ni Katibu Mkuu OR – UTUMISHI Juma Mkomi na wa pili kutoka kushoto ni Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama.



Washiriki wa mafunzo ya Mfumo mpya wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS) yaliyofanyika tarehe 4 – 6 Julai, 2023 jijini Dodoma wakisikiliza hotuba ya Waziri wa Nchi (Ofisi ya Rais) Menejimenti ya Utumishi wa Umma, George Simbachawene wakati wa kufunga mafunzo hayo.

SERIKALI YASISITIZA UTARATIBU WA WALIMU KUFANYA MITIHANI ILI KUAJIRIWA HAUTAWAGUSA WALIOKO KAZINI

Na Mwandishi wetu – Mwanza.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolf Mkenda amewatoa hofu walimu ambao tayari wako kwenye ajira kuhusu mfumo mpya wa ajira unaohusisha wahusika kufanya mitihani kwa kuwa hautawagusa wao.

Akizungumza tarehe 4 Julai, 2023 wakati akifungua mafunzo endelevu ya walimu kazini (Mewaka) kwa Maofisa Elimu Kata jijini Mwanza, Profesa Mkenda alisema mfumo huo wa mitihani ya kupima uwezo, ubora, weledi na ubunifu katika ufundishaji utawahusisha walimu wanaoingia katika ajira mpya na siyo walioko kazini.

Waziri Mkenda alitoa ufafanuzi huo kuondoa mkanganyiko na hofu miongoni mwa walimu walioko kazini kuhusu mfumo huo ambao ni miongoni mwa mapendekezo ya wadau kwenye seraya elimu unaolengakurejesha hadhi ya taaluma ya ualimu na kuondoa mtazamo wa sasa kuwa

fani hiyo ni chaguo la mwisho baada ya kukosa nyingine kwa wanafunzi wanaojiunga na vyuo hapa nchini.

Alisema Serikali inaendelea na mchakato wa kuchambua maoni ya wadau ambayo yatapitwa na kamati ya Makatibu Wakuu kabla ya kuwasilishwa kwenye Baraza la Mawaziri ambalo litamshauri Rais kuyaridhia na kuwa toleo la 2203 la Sera ya Elimu na mafunzo ya 2023.

Alisema kupitia sera hiyo, walimu waliopo kazini wataendelezwa kupitia kozi na mafunzo ya mara kwa mara huku wenye nia ya kujiendeleza wakiwezesha kutimiza malengo yao, dhumuni kuu ikiwa ni kufanya fani ya ualimu kuwa bora zaidi.

“Tutawalinda na tutawekeza kwa walimu waliopo kazini... ajira zao zitalindwa,” alisisitiza Profesa Mkenda.

Akizungunzia uimarishaji wa mafunzo na maendeleo ya kitaaluma, Waziri Mkenda aliwaagiza Maofisa Elimu Kata kusimamia vituo vya walimu na kutoa mrejesho wa mara kwa

maru wizarani wa namna ya kuvifanya kuwa bora Zaidi.

Akitoa taarifa ya mafunzo hayo, Mkurugenzi wa mafunzo ya walimu nchini, Huruma Mageni amesema jumla ya Maofisa Elimu Kata 2,384 nchini watapewa mafunzo hayo katika vituo viwili kimoja kikiwa Mwanza na kingine Iringa.

Ametaja kituo cha Mwanza kinajumuisha maofisa hao 1,175 kutoka mikoa ya Simiyu, Shinyanga, Arusha, Manyara, Singida, Tabora na Dodoma.

“Baada ya mafunzo haya kukamilika jumla ya walimu 45,979 na viongozi wa Elimu 3,412 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na Maofisa Elimu Kata 2,730 kutoka halmashauri 184 watakuwa wamejengewa uwezo wa kusimamia na kuendesha Mewaka katika shule na vituo vya walimu,” amesema.

Nao Maofisa Elimu Kata waliohudhuria mafunzo hayo waliishukuru Serikali kwa kutoa vishikwambi kwa walimu nchini wakisema vitawarahisishia utendaji kazi.



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolf Mkenda akizungumza wakati wa ufunguzi wa mafunzo endelevu ya walimu kazini (Mewaka) kwa Maofisa Elimu Kata kutoka mikoa saba jijini Mwanza.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na TEknolojia Prof. James Mdoe, akizungumza wakati wa Mafunzo kwa Maafisa Elimu Kata yanayotolewa na Wizara hiyo jijini Mwanza.



TSC NYASA YAWAPIGA MSASA WALIMU WA AJIRA MPYA

Na Mwandishi wetu – Nyasa.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Nyasa imeendesha Kikao kazi cha kuwajengea uwezo

walimu wa walioajiriwa hivi karibuni kuhusu Sheria, Kanuni na Taratibu mbalimbali za kiutumishi ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Kikao kazi hicho kilifanyika mwishoni mwa Mwezi Julai, 2023

katika Ukumbi wa Halmashauri Wilaya ya Nyasa ambapo Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Mthibiti Ubora wa Shule na Chama cha Walimu walishiriki.



WAZIRI KAIRUKI AWAONYA WATENDAJI WASIO WAADILIFU KATIKA KUWAHUDUMIA WALIMU

Na Mwandishi wetu - Dodoma

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Miko na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Angellah Kairuki, amewataka watendaji wanaoomba fedha walimu ili washughulikie madai yao kuacha tabia hiyo mara moja kwani ni kunyume na maadili ya utumishi wa umma na pia inasababisha mwalimu kukosa haki yake.

Alisema wapo baadhi ya watendaji ambao hutoa sharti la kupewa sehemu ya fedha atakazopata mwalimu husika ili ayashughulikie madai hayo.

Onyo hilo alilitoa tarehe 05 Julai, 2023 jijini Dodoma wakati akifungua mkutano wa maafisa utumishi wa halmashauri na watumishi wa Tume ya Utumishi

wa Walimu (TSC), ambapo alisema anapokea malalamiko mengi kutoka kwa walimu.

Alisema baadhi ya walimu pia humtumia ujumbe wa simu Rais, Samia Suluhu Hassan na kumuandikia barua kulalamikia kadhia hiyo.

“Kuna viongozi wanageuka kuwa miungu watu, wananyanyasa watumishi, wengine kuwatolea lugha zisizo na staha, kuwatukana na kuwatisha. Yaani mtu anadai haki yake halafu anawekewa mazingira ya kutoa rushwa. Vitendo kama hivi havikubaliki, atakayebainika tutaendelea kuchukua hatua,” alisema Kairuki.

Kairuki aliwataka watendaji hao kutimiza wajibu wao kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu na waache tabia ya kuwanyanyasa walimu. “Hakuna mtu aliyewalazimisha kufanya

hii kazi walitaka wenyewe, kama hamuwezi kuwahudumia watumishi wenzenu muondoke.”

“Labda wengine wana madai ya likizo ama uhamisho wanaenda kwa kamisheni za asilimia kwamba unadai milioni kadhaa ili uweze kupata ni lazima utoe hela, jamani hivi vitu haviwezekani ndugu zangu ni lazima vifike mwisho,” alisema.

Aliongeza kuwa, wapo walimu wa ajira mpya ambao walioripoti kazini Juni mwaka huu lakini hadi kufikia mwezi Julai walikuwa hawajalipwa stahiki zao, aliamuru maafisa utumishi kuhakikisha wanawalipa kwa wakati.

Naye Katibu wa TSC, Paulina Mkwama aliishukuru Serikali kwa kuahidi kutoa vitendea kazi ikiwemo magari 16 na kompyuta 159 kwa watendaji wa Tume hiyo.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Miko na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Angellah Jasmine Kairuki (kulia) akiteta jambo na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama wakati wa kufungua mafunzo ya Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Watumishi yaliyowahusisha watumishi wa TSC ngazi ya wilaya na Maafisa Utumishi kutoka Halmashauri zote nchini tarehe 05 Julai, 2023 jijini Dodoma.



Washiriki wa mafunzo ya Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Watumishi ujulikanao kama Human Capital Information Management System (HCIMS) yaliyowahusisha watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ngazi ya Wilaya na Maafisa Utumishi kutoka Halmashauri zote nchini tarehe 05 Julai, 2023 jijini Dodoma wakiwa kwenye mafunzo.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Angellah Jasmine Kairuki (katikati waliokaa) akiwa katika picha wa pamoja na baadhi ya washiriki wa mafunzo ya Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Watumishi yaliyowahusisha watumishi wa TSC ngazi ya wilaya na Maafisa Utumishi kutoka Halmashauri zote nchini tarehe 05 Julai, 2023 jijini Dodoma. Pichani, wa pili kutoka kulia ni Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI anayeshughulikia elimu, Dkt. Charles Msonde na wa pili kutoka kushoto ni Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS



TUME YA UTUMISHI WA WALIMU

**MKATABA WA HUDUMA
KWA MTEJA**

1.0 DIRA, DHIMA NA MAADILI YETU

1.1 Dira

Kuwa Taasisi inayoongoza katika kuwezesha Uwajibikaji na Uadilifu katika Utumishi wa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari ”

1.2 Dhima

“Kuhakikisha Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari wanapata huduma bora kuhusu masuala ya Ajira, kupandishwa vyeo na kukuza Maadili”

1.3 MAADILI YETU

Ili kuhakikisha uwepo wa utoaji huduma ulio bora, Tume ya Utumishi wa Walimu itatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia yafuatayo:-

i. **Uadilifu**

Tunatoa huduma kwa uaminifu na kuheshimu wateja wetu;

ii. **Haki**

Tunatoa huduma zetu kwa usawa;

iii. **Usiri**

Tunatoa huduma kwa kuzingatia utunzaji wa taarifa za wateja na kuzitumia kwa malengo yaliyokusudiwa tu,

iv. **Uwajibikaji**

Tunawajibika kwa matendo yetu kwa huduma tunazozitoa;

v. **Uzingatiaji wa Sheria**

Tunatoa huduma zetu kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zilizowekwa;

vi. **Ushirikiano**

Tunafanya kazi kwa pamoja ili kufikia malengo ya Taasisi yetu.

2.0 MADHUMUNI YA MKATABA

Madhumuni ya Mkataba huu ni kuufahamisha Umma kuhusu huduma na viwango vya huduma zinazotolewa na Tume. Pia, utasaidia kujenga imani na kuboresha mahusiano kati ya Tume na wateja wake kwa kuzingatia ubora na viwango vya huduma vinavyotarajiwa kutoka kwetu, na kuhakikisha kwamba haki za Wateja zinapewa kipaumbele katika huduma zetu. Aidha, Mkataba huu unalenga kumuwezesha mteja kutoa mrejesho wa malalamiko, maoni au mapendekezo kutokana na huduma tunazozitoa.

3.0 WATEJA WETU

Tume ya Utumishi wa Walimu inatoa huduma zake kwa wateja wafuatao:-

- i. Ofisi ya Rais Ikulu;
- ii. Walimu;
- iii. Wanafunzi wa shule;
- iv. Bunge;
- v. Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- vi. Tume ya Utumishi wa Umma;
- vii. Mifuko ya Hifadhi ya Jamii;
- viii. Wadau wa maendeleo;
- ix. Watoa huduma Asasi za Kiraia;
- x. Vyombo vya Habari;
- xi. Watu wenye mahitaji maalum; na
- xii. Wananchi.

4.0 HUDUMA ZETU

Tume ya Utumishi wa Walimu inatoa huduma zifuatazo;

- i. Usajili wa Walimu;
- ii. Kuthibitisha Walimu Kazini;
- iii. Upandishwaji vyeo Walimu;
- iv. Maadili na Nidhamu ya Walimu;
- v. Vibali vya kustaafu Walimu;
- vi. Taarifa mbalimbali za Tume;
- vii. Takwimu mbalimbali kuhusu Walimu;
- viii. Elimu na Ushauri wa Kitaalamu; na
- ix. Huduma Nyinginezo.

5.0 VIWANGO VYA HUDUMA ZETU

5.1 Ajira, Uthibitisho Kazini na Kibali cha Kustaafu

- i. Tutatoa barua ya ajira ya mwalimu ndani ya **siku 14** baada ya uhakiki kukamilika; na
- ii. Tutatoa Uthibitisho wa kazi kwa mwalimu ndani ya siku **90** baada ya **miezi tisa (9)** ya utumishi.
- iii. Tutatoa Kibali cha Mwalimu kustaafu ndani ya **miezi sita (6)** kabla ya tarehe ya kustaafu

5.2 Kutoa Uamuzi na Rufaa

- i. Tutatoa Uamuzi wa Shauri la nidhamu ndani ya **siku 165** baada ya kuanzishwa; na
- ii. Tutatoa Uamuzi wa rufaa ndani ya **siku 90** baada ya kupokea vielelezo.

5.3 Tutatoa miongozo mbalimbali ya masuala ya Utumishi wa walimu ndani ya siku 1 ya kazi. Miongozo hiyo ni:

- i. Mwongozo wa Usimamizi wa Maadili na Nidhamu ngazi ya shule;
- ii. Mwongozo wa hatua za Nidhamu na Rufaa kwa walimu; na
- iii. Mwongozo kuhusu msauzaji wa ajira na maendeleo ya walimu.

5.4 Kutoa Taarifa mbalimbali za Tume

- i. Tutatoa taarifa za Mirathi kwa Walimu waliofariki kabla ya Julai 1, 2004 ndani ya **siku 14** za kazi baada ya kupokea maombi;
- ii. Tutatoa taarifa za Mafao ya kustaafu kwa Walimu waliostaafu kabla ya Julai 1, 2004 ndani ya **siku 14** za kazi baada ya kupokea maombi;
- iii. Tutatoa taarifa Utekelezaji wa Malalamiko ya walimu ndani ya **siku 14** za kazi baada ya kupokelewa;
- iv. Tutatoa taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ndani ya **siku 15** baada ya kila robo mwaka;
- v. Tutatoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Tume ndani ya **siku 15** baada ya kukamilika kwa robo mwaka;
- vi. Tutatoa taarifa Manunuzi ndani ya **siku 15** baada ya kukamilika kwa robo mwaka; na
- vii. Tutatoa taarifa za kiutumishi ndani ya siku **siku 15** baada ya kukamilika kwa robo mwaka.

5.5 Kutatoa elimu na ushauri kitaalam kuhusu:-

- i. Maadili, Miiko ya Utumishi, Haki na Wajibu wa Mwalimu katika **kila robo** mwaka;
- ii. Masuala ya Ajira na Maendeleo ya Walimu kila inapohitajika; na
- iii. Mpango wa mafunzo kwa walimu **kila robo** mwaka.

5.6 Huduma nyinginezo

- i. Tutatoa malipo kwa mzabuni ndani ya **siku 14** za kazi baada ya huduma kukamilika;
- ii. Tutatoa tuzo kwa mzabuni ndani ya **siku 7** baada ya Uamuzi wa Bodi ya wazabuni kutolewa;
- iii. Tutatoa mrejesho wa malalamiko yanayohusu ajira, mashauri ya nidhamu na rufaa za walimu ndani ya **siku 14** za kazi baada ya kupokelewa;
- iv. Tutatoa majibu ya hoja za ukaguzi wa matumizi ya fedha ndani ya **siku 21** za kazi baada ya hoja kupokelewa;
- v. Tutatoa mrejesho wa malalamiko ya wanafunzi dhidi ya walimu ndani ya **siku 14** za kazi baada ya kupokelewa;
- vi. Tutakiri kupokea barua ndani ya **siku 3** za kazi;
- vii. Tutajibu barua za kawaida ndani ya **siku 5** na barua pepe ndani ya **siku 1**; na
- viii. Tutapokea simu ya ofisi ndani ya **miito mitatu (3)**.

6.0 WAJIBU WA TAASISI KWA MTEJA

Tume ina wajibu ufuatao kwa Wateja wake: -

- i. Kutoa huduma kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu;
- ii. Kutoa mrejesho wa malalamiko/rufaa ya mteja;
- iii. Kumsikiliza na kumjali mteja;
- iv. Kutumia lugha ya staha wakati wa kumhudumia mteja;
- v. Kutoa taarifa sahihi na kwa wakati;
- vi. Kutunza siri za Mteja;
- vii. Kutoa huduma bora bila upendeleo;

7.0 HAKI NA WAJIBU WA MTEJA

7.1 Haki za Mteja

- i. Kusikilizwa na kupata taarifa mbalimbali kwa mujibu wa Sheria, kanuni na taratibu;
- ii. Kuwa na faragha ya kutunziwa Siri;

- iii. Kuhudumiwa kwa heshima;
- iv. Kupewa taarifa kuhusu maamuzi na sababu za uamuzi wa Mashauri ya Nidhamu na rufaa.; na
- v. Kukata rufaa kwa kufuata taratibu zilizowekwa;

7.2 Wajibu wa Mteja

- i. Kujitambulisha na kutoa njia sahihi za mawasiliano pale zinapohitajika;
- ii. Kutoa taarifa zinazohitajiwa kwa usahihi, wakati na uwazi;
- iii. Kuheshimu na kuwaamini watoa huduma;
- iv. Kuepuka vishawishi vinavyoashiria rushwa na uvunjifu wa amani; na
- v. Kuwasilisha malalamiko kwa njia zilizo sahihi.

8.0 MREJESHO WA UTOAJI HUDUMA

Tunawakaribisha wateja na wadau wetu kutoa mrejesho kuhusu utoaji wa huduma za TSC kulingana na viwango vilivyoainishwa kwenye Mkataba huu. Mrejesho kuhusu huduma zinazotolewa unaweza kuwa wa Maoni, mapendekezo, malalamiko au pongezi na unaweza kutolewa kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na Sanduku la Maoni, barua, simu, barua pepe, ana kwa ana, tovuti, nukushi, mitandao ya kijamii, kituo cha huduma kwa mteja na dawati la malalamiko lililopo katika Ofisi zetu.

9.0 UTAMBULISHO WA TAASISI NA NJIA ZA MAWASILIANO

Makao Makuu ya Tume ya Utumishi wa Walimu yapo Jijini Dodoma. Tume ina ofisi katika Wilaya zote **139** katika Mikoa **26** Tanzania Bara, Ofisi zetu zipo wazi kuanzia saa 1:30 Asubuhi hadi saa 9:30 Alasiri (Jumatatu hadi Ijumaa).

Ili kuweza kuwasiliana nasi unaweza kutumia anuani zilizopo katika Mkataba huu kwa anuani zifuatazo:-

Makao Makuu

Ofisi ya Rais,
Tume ya Utumishi wa Walimu,
S. L. P 353,
Mtaa wa Mtendeni,
Jengo la LAPF zamani; Ghorofa ya 2 & 3,
41105 DODOMA – TANZANIA.

Simu: +255-262-322-462-4

Barua-pepe: secretary@tsc.go.tz

Tovuti: www.tsc.go.tz

WALIMU WAIPONGEZA TSC BUKOMBE KWA KUWAPANDISHA VYEO WALIMU 503

**Na Mwandishi Wetu -
Bukombe.**

Walimu wilayani Bukombe wameipongeza Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wilayani hapo kwa kupandisha

madaraja walimu 503 wa shule za msingi na sekondari ambapo wote wamepata mishahara ya vyeo vipya.

Pongezi hizo zilitolewa tarehe 3 Julai, 2023 wakati wa kikao cha TSC na walimu wa Shule za Msingi Azimio na Ushirombo chapo kiliwahusisha watendaji

mbalimbali wa Halmashauri hiyo ambao ni Mkurugenzi wa Halmashauri, Maafisa Elimu, Afisa Utumishi, Wathibiti Ubora wa Shule kutoka Wilaya ya Bukombe.

Naye Mkurugenzi Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Lutengano Mwalwiba aliwapongeza walimu kwa kazi nzuri wanayofanya ya kufundisha wanafunzi kitu kinachosaidia Wilaya hiyo kuendelea kupiga hatua katika maendeleo ya elimu.



WAZIRI SIMBACHAWENE AKEMEA WATUMISHI WANAJOJHUSISHA NA RUSHWA

Na Mwandishi wetu - Dodoma

Waziri wa Nchi (Ofisi ya Rais) Menejimenti ya Utumishi wa Umma, George Simbachawene amewataka Maafisa utumishi nchini kufanya kazi kwa weledi na uadilifu na kuepukana na vitendo vya rushwa ambavyo vinarudisha nyuma juhudi za maendeleo nchini.

Simbachawene alisema hayo tarehe 6 Julai, 2023 wakati akifunga mafunzo kwa watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) na maafisa utumishi wa halmashauri za Tanzania Bara jijini hapa.

Akizungumza katika mafunzo hayo yaliyoandaliwa na TSC kufundisha jinsi ya kutumia mfumo mpya wa Taarifa Shirikishi za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS), Simbachawene alisema baadhi ya maafisa utumishi wanapokea rushwa kati ya Sh5 milioni hadi Sh10 milioni ili watoe ukuu wa vitengo na idara.

"Kwa maafisa utumishi huko kuna changamoto, rushwa ni nyingi," alisema Simbachawene.

Alisema ujio wa mfumo huo utakuwa na taarifa zote na rahisi kuwabaini maafisa wanaowateua watendaji baada ya kupokea rushwa.

"Wako watumishi huko wilayani, wanatuambia kabisa, pale kwetu siwezi kuteuliwa hata kama nina sifa, labda mniteue ninyi moja kwa moja. Sasa sisi Wizara ya Utumishi hatuteui tu watu, kuna mamlaka za ajira, lazima zifanye michakato, lakini haifanyiki kwa sababu ya rushwa," alisema Simbachawene.

Pia, alisema kuna changamoto ya watumishi kukaimishwa madaraka kwa muda mrefu, hali inayosababishwa na



Waziri wa Nchi (Ofisi ya Rais) Menejimenti ya Utumishi wa Umma, George Simbachawene akiongea na Watumishi wa TSC na maafisa utumishi kutoka Halmashauri zote nchini wakati akifunga mafunzo ya Mfumo mpya wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS) tarehe 6 Julai, 2023 jijini Dodoma.

baadhi ya maafisa utumishi wanaotaka kupatiwa rushwa ndipo wapendekeze watumishi wengine.

"Hamuanzishi mchakato kwa sababu rushwa imewajaa. Nayasema haya mimi ni mbunge miaka 20, ni Waziri niliyepita wizara nyingi, wengine mko nao huko, ni jamaa zetu, ni ndugu zetu," alisema.

Hata hivyo, alisema kuanzia sasa, wakibaini kuna mtumishi mwenye sifa lakini hajaanzishiwa mchakato au kupandishwa cheo, ofisa utumishi wa halmashauri husika atachukuliwa hatua.

Alisema kwa wanaofanya kazi halmashauri mchakato mara zote huanzia huko na kwenda Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI).

Simbachawene alisema maafisa hao hawafuati utaratibu huo, badala yake wanaficha taarifa za watumishi wenye sifa kwa makusudi ili wawapandishe waliowapa rushwa.

"Jamani hii nchi tunaiua wenyewe, huko kwenye mitandao mnatupiga kweli wakati ninyi

ndio waharibifu," alisema Simbachawene na kuwataka wabadilike na wafanye kazi kwa weledi.

Hata hivyo, alisema maafisa utumishi wanakabiliwa na changamoto mbalimbali, ikiwamo ya ukosefu usafiri, wakati mwingine huchangisha fedha kutoka kwa watumishi kwa madai ya kwenda Ofisi ya Rais UTUMISHI kushughulikia matatizo ya watumishi wa halmashauri zao.

Katibu Mkuu (Ofisi ya Rais) Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Juma Mkomi alisema kama itafanyika tathimini ya watumishi wanaopeleka malalamiko kwenye ofisi yake, wengi ni walimu.

"Ni imani yetu ujio wa mfumo huu utatusaidia kutatua changamoto za walimu. Si kwa mfumo tu, bali utashi pia," alisema Mkomi.

Mafunzo hayo yalilenga kuwapatia uelewa watumishi wa TSC na kuwawezesha kupata dirisha la kuingia kwenye mfumo huo wa taarifa za watumishi wa Umma kwa ajili ya kushughulikia changamoto za walimu.



Waziri wa Nchi (Ofisi ya Rais) Menejimenti ya Utumishi wa Umma, George Simbachawene akiongea na Watumishi wa TSC na maafisa utumishi kutoka Halmashauri zote nchini wakati akifunga mafunzo ya Mfumo mpya wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS) tarehe 6 Julai, 2023 jijini Dodoma.

Katibu Mkuu Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Juma Mkomi akitoa neno la kumkaribisha Waziri Simbachawene ili afunge mafunzo ya Mfumo mpya wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS) tarehe 6 Julai, 2023 jijini Dodoma.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akitoa maelezo mafupi kwa Waziri wa Nchi (Ofisi ya Rais) Menejimenti ya Utumishi wa Umma, George Simbachawene wakati wa kufunga mafunzo ya Mfumo mpya wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS) tarehe 6 Julai, 2023 jijini Dodoma.



Washiriki wa mafunzo ya Mfumo mpya wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS) yaliyofanyika tarehe 4 – 6 Julai, 2023 jijini Dodoma wakisisikiliza hotuba ya Waziri wa Nchi (Ofisi ya Rais) Menejimenti ya Utumishi wa Umma, George Simbachawene wakati wa kufunga mafunzo hayo.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene (katikati waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na washiriki wa mafunzo ya Mfumo mpya wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS) wakati wa kufunga mafunzo hayo tarehe 6 Julai, 2023. Pichani, wa pili kutoka kulia ni Katibu Mkuu Ofisi ya Rais UTUMISHI, Juma Mkomi na wa pili kutoka kushoto ni Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama.

TSC NGORONGORO YATEMBELEA SHULE YA SEKONDARI NGORONGORO

Na Mwandishi wetu - Dodoma

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Ngorongoro imefanya ziara katika shule ya Sekondari ya wasichana Ngorongoro (Ngorongoro Girls) kwa lengo la kutoa elimu juu ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu pamoja na kushughulikia masuala mbalimbali ya kiutumishi.



SERIKALI YAJIPANGA KUMALIZA KERO NA MALALAMIKO YA WALIMU

Na. Mwandishi Wetu – Dodoma.

Serikali imejipanga kumaliza kero na malalamiko mbalimbali yanayowakabili walimu kwa kuhakikisha kila mwalimu anapatiwa haki yake kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu za kiutumishi.

Miongoni mwa kero kubwa ambazo serikali imejipanga kuzimaliza ni kucheleweshwa kupandishwa vyeo, kupandishwa madaraja bila kuzingatia utaratibu jambo linalosababisha kutofautiana kwa vyeo kwa walimu wa kundi rika moja (walioanza kazi pamoja na wenye sifa sawa) na kujirudia kwa madaraja (mwalimu kupandishwa cheo katika daraja lile lile alilionalo).

Malalamiko mengine ni walimu wanaopanda vyeo



Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI) anayeshughulikia elimu, Dkt. Charles Msonde akizungumza na watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakati wa mafunzo ya Usimamizi wa Mfumo wa Usiamizi wa Taarifa za Watumishi ujulikanao kwama Human Capital Information Management System (HCIMS) tarehe 04 Julai, 2023 katika Ukumbi wa Jeshi la Zimamoto jijini Dodoma.



Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama akitoa neno wakati wa mafunzo ya Usimamizi wa Mfumo wa Usiamizi wa Taarifa za Watumishi ujulikanao kwama Human Capital Management Information System (ICMIS) yaliyowahusisha watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kutoka wilaya zote za Tanzania Bara yaliyofanyika tarehe 04 Julai, 2023 katika Ukumbi wa Jeshi la Zimamoto jijini Dodoma.

pamoja kuidhinishwa barua za kupanda vyeo kwa tarehe tofauti kwa sababu za kimfumo, kucheleweshwa kubadilishiwa cheo baada ya kujiendeleza kielimu pamoja na madai ya malimbikizo ya mishahara, likizo na uhamisho.

Hayo yamebainishwa na Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa anayeshughulikia elimu, Dkt. Charles Msonde tarehe 4 Julai, 2023 wakati akiongea na watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwenye mafunzo ya Usimamizi wa Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Watumishi ujulikanao kwama Human Capital Management Information System (UCMIS) jijini Dodoma.

“Kufuatia malalamiko hayo sisi watendaji tuliopewa dhamana ya

SERIKALI YA JIPANGA KUMALIZA KERO NA MALALAMIKO YA WALIMU

kuwasimamia walimu tumekaa na kukubaliana kwamba kuna haja ya kutafuta ufumbuzi wa changamoto hizi ili kila mwalimu apate haki yake na afanye kazi kwa amani. Hivyo, tumeanza zoezi la kukusanya taarifa za mwalimu mmoja mmoja ili kubaini changamoto za kiutumishi alizonazo. Na kazi ya kukusanya taarifa hizo tumewapa ninyi watendaji wa TSC, mzichambue na kutupa mapendekezo ya nini kifanyike kwa kila mwalimu," alisema Dkt. Msonde.

Kiongozi huyo aliwataka watumishi wa TSC kufanya kazi hiyo kwa makini huku akisisitiza kuwa baada ya zoezi hilo kukamilika endapo atatokea mwalimu mwenye malalamiko ambaye taarifa zake hazikutolewa Serikali itachukua hatua kali kwa mtendaji atakayekuwa amehusika na uzembe huo.

"Na kama kuna mwalimu ataleta malalamiko haya haya tunayoyafanyia kazi sasa na tukagundua afisa wa TSC au Afisa Utumishi wa Halmasahauri hamkufanya kazi yenu vizuri hatutawavumilia. Tumewapa muda wa kutosha, kila mtu apitie taarifa za mwalimu mmoja mmoja



Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Singida ambaye alichaguliwa kuwa mwenyekiti katika mafunzo hayo, Mwl. Fundikira James akitoa neno la kumkaribisha Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI) anayeshughulikia elimu, Dkt. Charles Msonde ili azungumze na washiriki wa mafunzo.

kwenye wilaya yake mtuletee kazi iliyokamilika. Hatutaki ulete kitu chochote chenye makosa," alisisitiza.

Pamoja na hayo, Dkt. Msonde aliwataka watumishi hao kuwahudumia walimu kwa upendo na kuwatia moyo badala ya kuwanyanyasa jambo ambalo linawavunja moyo na kuwakatisha tamaa ya utendaji kazi.

Kwa upande wake Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama alisema mafunzo hayo yanayotolewa na watendaji kutoka Ofisi ya

Rais – UTUMISHI yanalenga kuwajengea uwezo watumishi wa TSC ili waweze kutumia mfumo huo katika kuwahudumia walimu ikiwa ni moja ya mikakati ya Serikali ya kutafuta ufumbuzi wa changamoto zinazowakumba walimu.

"Tunawashukuru sana Ofisi ya Rais – UTUMISHI kwa kukubali watumishi wetu kupata mafunzo haya ambayo yatawawezesha kutumia mfumo huu wa kiutumishi katika kushughulikia masuala mbalimbali ya kiutumishi yanayowahusu walimu. Bila shaka, baada ya kuanza utekelezaji wa haya tunayojifunza tutakuwa tumewasaidia walimu kupata huduma zao kwa ubora na kwa wakati zaidi kuliko ilivyo sasa," amesema Nkwama.

Pia, aliishukuru Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa kuendelea kuisaidia Tume hiyo kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kuhakikisha changamoto mbalimbali zinazowakabili walimu zinatatuliwa kwa haraka na walimu wanaendelea kufanya kazi katika mazingira ya tulivu.



Mkurugezi wa Idara ya Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu TSC, Mwl. Fatuma Muya akitoa neno wakati wa mafunzo ya Usimamizi wa Mfumo wa Usiamizi wa Taarifa za Watumishi.



Washiriki wa mafunzo ya Usimamizi wa Mfumo wa Usiamizi wa Taarifa za Watumishi ujulikanao kwama Human Capital Information Management System (HCIMS) yaliyowahusisha watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kutoka wilaya zote za Tanzania Bara wakiwa kwenye mafunzo.

TSC BUTIAMA YATOA ELIMU KWA WALIMU KUHUSU UFAFANUZI WA KANUNI ZA MAADILI NA UTENDAJI KAZI KATIKA UTUMISHI WA WALIMU



Afisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Butiama, Bi. Regina Donatus Kinabo akitoa ufafanuzi wa kanuni za maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu kwa Wakuu wa shule 21 na Maafisa Elimu kata 18 katika Ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Butiama, tarehe 13 Julai, 2023.

**WAZIRI SIMBACHAWENE AWATAKA VIONGOZI
KUSIKILIZA MALALAMIKO YA WATUMISHI**



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene

**Na Mwandishi wetu –
Mpwapwa.**

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene amewataka viongozi wa ngazi za Wilaya na Halmashauri zote nchini kujenga utamaduni wa kusikiliza

na kufanyia kazi malalamiko mbalimbali ya Watumishi wa Umma huku akisema kiu yake ni kuona watumishi hao wakifurahia kuwa Watumishi wa Wananchi.

Waziri Simbachawene ametoa kauli hiyo wakati akizungumza na Watumishi wa Umma wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa mkoani Dodoma, ambapo amesema yeye kama kiongozi anatambua watumishi

wanakabiliwa na changamoto lukuki na hawana sehemu ya kusemea.

Amesema watumishi waliokata tamaa hawawezi kutoa huduma bora kwa wananchi huku akisisitiza kuwa hali hiyo imekuwa ikiwaumiza wananchi na kuifanya serikali iliyopo madarakani kuchukiwa kwa matatizo yao kutopatiwa ufumbuzi. Amefafanua kuwa anataka kuona watumishi wa umma wakipata stahiki zao lakini na wao wakitekeleza majukumu yao ipasavyo.

Kufuatia hatua hiyo, Mhe. Simbachawene amewataka Makatibu Tawala wa Wilaya nchini ambao ndio wakuu wa utumishi wa umma katika ngazi ya wilaya kutekeleza majukumu yao kwa kusikiliza vilio na malalamiko ya watumishi walio chini yao. "Watumishi waliochukia na wenye malalamiko hawawezi kuleta matokeo chanya ambayo Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan anakusudia, hivyo Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi wa Halmashauri na Katibu Tawala wa Wilaya shughulikieni matatizo ya watumishi" amesisitiza Mhe. Simbachawene.

Aidha, Mhe. Simbachawene amesema Watumishi wa Umma wanaokiuka misingi ya utumishi wa umma akitolea mfano ulevi kazini ni vizuri wakawa wanaonywa kabla ya kuadhibiwa ikizingatiwa sasa hivi waajiriwa wengi ni vijana sana hivyo wanachohitaji ni malezi pekee.

Katika zoezi hilo la kusikiliza malalamiko ya watumishi, miongini mwa malalamiko yaliyotewa kwa wingi na watumishi hao ni kuchelewa kulipwa malimbikizo yao ya mishahara, kupandishwa madaraja, kuchelewa kulipwa fedha za uhamisho pamoja na kubambikiwa mikopo.

Na Mwandishi wetu – Kakonko.

**TSC KAKONKO YAWAFIKIA
WALIMU KATA YA RUGENGE**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kakonko imefanya kikao kazi na Walimu kutoka katika Shule za Kata ya Rugenge ambacho kililenga kutoa elimu juu ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na utendaji

Kazi katika Utumishi wa Walimu, kusikiliza na kutatua changamoto za walimu pamoja na kuhimiza utendaji kazi wa kila siku.

Kikao kazi hicho kilifanyika

tarehe 28 Julai, 2023 na kilihudhuriwa na Afisa Elimu Msingi na Chama cha Walimu wilayani hapo ambapo walimu 55 wa shule za Msingi na Sekondari walihudhuria.



Kikao kazi cha Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kakonko na walimu wa kutoka shule za Kata ya Rugenge kikiwa kinaendelea.



Katibu wa Kamati ya Ukaguzi wa Ndani ya TSC, Laurence Chankan akitoa neno la utangulizi wa ufunguzi wa mafunzo ya Kamati hiyo tarehe 12 Juni, 2023 jijini Dodoma.



Mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi wa Ndani ya TSC ambaye pia ni Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu, Mwl. Fatuma Muya akitoa neno la shukari wakati wa ufunguzi wa mafunzo hayo tarehe 12 Juni 2023 katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kivete jijini Dodoma.



Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Wajumbe wa Kamati ya Ukaguzi wa Ndani na Wajumbe wa Menejimenti ya TSC wakati wa ufunguzi wa mafunzo hayo uliofanyika tarehe 12, Juni 2023 jijini Dodoma. Wengine waliokaa ni, Kaimu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Upendo Werema (pili kutoka kushoto), Katibu wa Kamati hiyo, Lawrence Chankan (wa pili kutoka kulia), Mjumbe wa Kamati hiyo, Mwl Fatuma Muya (wa kwanza upande wa kulia) na Mwezeshaji wa Mafunzo hayo, Alphonse Muro (wa kwanza kushoto).



Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Sekretarieti ya Kamati ya Ukaguzi wa Ndani wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya Kamati ya Ukaguzi wa Ndani ya TSC uliofanyika tarehe 12, Juni 2023 jijini Dodoma. Wengine waliokaa ni, Kaimu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Upendo Werema (pili kutoka kushoto), Katibu wa Kamati hiyo, Lawrence Chankan (wa pili kutoka kulia), Mjumbe wa Kamati hiyo, Mwl. Fatuma Muya (wa kwanza upande wa kulia) na Mwezeshaji wa Mafunzo hayo, Alphonse Muro (wa kwanza kushoto).



Washiriki wa Mafunzo ya Kamati ya Ukaguzi wa Ndani ya TSC wakivwa kwenye mafunzo.

SERIKALI YASISITIZA KUMALIZA MADAI YA WALIMU

Na Mwandishi wetu – Manyoni.

Serikali inatarajia kuwalipa kumaliza changamoto za walimu ikiwa ni pamoja na kuwalipa stahiki zao.

Akizungumza na walimu wakuu, watibu elimu kata na maafisa elimu waliokuwa katika mafunzi ya kuwajengea uwezo wa matumizi ya vifaa vilivyoboreshwa kupitia mradi

wa BOOST yaliyofanyika wilayani Manyoni mkoani Singida, Naibu katibu mkuu TAMISEMI Dkt. Charles Msonde amesema serikali inatambua mchango mkubwa wa walimu katika kutoa elimu bora nchini hivyo malipo yao yatalipwa katika mwaka wa fedha 2023/2024 unaoanza.

Dkt. Msonde amewataka walimu kujituma katika kufundisha huku akiwapa moyo

katika kutekeleza majukumu yao.

Aidha ametembelea kujionea hali ya ujenzi wa vyumba vya madarasa na mabweni shule hiyo ya Sekondari Mwanzi ambapo ameipongeza kwa kufikia hatua nzuri sanjari na kutaka kuongeza nguvukazi kwenye ujenzi wa mabweni kutokana na umuhimu wa siku chache zijazo watakapoanza kupokea wanafunzi.



Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI) anayeshughulikia elimu, Dkt. Charles Msonde.



MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz